

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
BARAZA LA MITIHANI  
MTIHANI WA UALIMU DARAJA LA A

662 UTAFITI WA KIELIMU, UPIMAJI NA TATHMINI

Muda: Saa 3

Jumatano, Oktoba 12, 2005 Asubuhi.

Maelekezo

1. Karatasi hii ina sehemu A, B na C.
2. Jibu maswali yote katika sehemu A, maswali mawili (2) kutoka sehemu B na swali moja (1) kutoka sehemu C.
3. Swali la kumi na moja (11) ni la lazima kwa kila mtahiniwa.
4. Mashine za hesabu za elektroniki haziruhusiwi katika chumba cha mtihani.
5. Simu za mkononi haziruhusiwi katika chumba cha mtihani.
6. Andika Namba yako ya Mtihani katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha kujibua.

**SEHEMU A (alama 36)**

Jibu maswali yote katika sehemu hii.

1. Bainisha mambo **manne** (4) yanayoonesha umuhimu wa matokeo ya upimaji kwa shule.
2. Tofautisha aina kuu **mbili** (2) za maswali ya insha.
3. Eleza aina **mbili** (2) za upungufu wa maswali ya kuoanisha.
4. Eleza kwa kifupi maana ya Jedwali la Kutahinia.
5. Eleza kwa kifupi tofauti iliyopo kati ya alama ghafi na alama sanifu.
6. Fafanua kwa kifupi dhana zifuatazo kama zinavyotumika katika kutafsiri alama za wanafunzi.
  - (a) Mchirizo hasi. ↗
  - (b) Mchirizo chanya. ↘
7. Kwa kutumia alama za wanafunzi zifuatazo: 15, 12, 20, 35, 45, 25, 35, 41; eleza maana ya dhana zifuatazo.
  - (a) Modi.
  - (b) Alama kati.
  - (c) Wastani.
  - (d) Mfiko.
8.
  - (a) Eleza maana ya sampuli ya utafiti.
  - (b) Bainisha njia mbili za kupata sampuli za utafiti.
9. Orodhesha sifa **tatu** (3) za bunio la utafiti.

**SEHEMU B (alama 40)**

Jibu maswali **mawili** (2) katika sehemu hii.

10. Jadili sababu **nne** (4) zinazobainisha umuhimu wa kurekebisha alama za wanafunzi.
11. Zifuatazo ni alama walizopata wanafunzi wa Darasa la VII katika jaribio la somo la Kiswahili.

Mwanafunzi	A	B	C	D	E	F	G	H	I	J	K	L	M	N	O
Alama	30	45	60	60	50	55	48	70	30	60	72	60	71	63	36

- (a) Kutokana na alama zilizoko katika jedwali la hapo juu, tafuta:
  - (i) mfiko.
  - (ii) wastani.
  - (iii) achano sanifu.
- (b) Rekebisha alama za wanafunzi **A** na **K** iwapo wastani ni 50 na achano sanifu ni 10.

12. Maswali mengi ya majaribio katika shule za msingi ni yale ya kuchagua jibu sahihi. Eleza kwa ufasaha manufaa manne (4) na aina mbili (2) za upungufu wa maswali ya aina hiyo.
13. Fafanua ngazi sita (6) katika maeneo ya utambuzi.

**SEHEMU C (alama 24)**

Jibu swali moja (1) kutoka sehemu hii.

14. Kuna hatua za msingi ambazo mwalimu bora anapaswa kuzifuata katika kupima maendeleo ya wanafunzi wake. Jadili kwa ufasaha hatua hizo.
15. Mara nyingi baada ya mtafiti kukamilisha hatua ya kukusanya taarifa mbalimbali anatakiwa aandike ripoti juu ya utafiti alioufanya. Chambua hatua muhimu atakazofuata katika kuandika ripoti ya utafiti huo.
16. Kama utateuliwa na Mwalimu Mkuu wa shule yako kutoa mada ya kutathmini somo, fafanua hatua utakazowashauri walimu wenzako kuzifuata ili waweze kufanya tathmini nzuri ya masomo yao.

$$\begin{array}{r} 458 \\ 144 \\ \hline 602 \\ 81 \\ \hline 683 \\ 258 \\ \hline 939 \\ 289 \\ \hline 1228 \\ 320 \\ \hline 1548 \end{array}$$

- Malengo talipokusudiwa kama  
 - lengo kuu  
 - lengo mahsusi

- Ushirikiano wa wanafunzi  
 ni wa nanna gani kabika majadili

- Masoezi na kazi za wanafunzi  
 - kusahihisha kazi → wanaozi wa wanafunzi

- Matokeo ya kazi hizo za wanafunzi  
 - kufanya tathmini hiyo

$$\begin{array}{r} 54 \\ -30 \\ \hline 24 \end{array}$$

$$\begin{array}{r} 54 \\ 36 \\ \hline 18 \end{array}$$

$$\begin{array}{r} 24 \\ \times 24 \\ \hline 96 \\ 480 \\ \hline 576 \end{array}$$

$$\begin{array}{r} 576 \\ 2 \\ \hline 1152 \end{array}$$

$$\begin{array}{r} 1152 \\ 1352 \\ \hline 2704 \end{array}$$

$$\begin{array}{r} 398 \\ +324 \\ \hline 716 \\ 81 \\ \hline 797 \\ 36 \\ \hline 833 \\ 17 \\ \hline 850 \\ 144 \\ \hline 994 \\ 81 \\ \hline 1075 \\ 869 \end{array}$$

$$\begin{array}{r} 576 \\ 289 \\ \hline 865 \\ 324 \\ \hline 1189 \end{array}$$

$$\begin{array}{r} 324 \\ 81 \\ \hline 405 \\ 36 \\ \hline 441 \\ 10 \\ \hline 451 \end{array}$$